TRC
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

# RELI NA MATUKIO GAZETI

Kila Mwezi



Novemba 01, 2019


Gazeti la Reli | Toleo Namba 3 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

## SHIRIKA LA RELI TANZANIA NA CLOUDS MEDIA GROUP WAADHIMISHA MIAKA 20 YA MWL. NYERERE



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa, timu ya CMG, na baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya Yapi Merkezi wakiwa katika picha ya pamoja katika handaki namba 2 linaloendelea kujengwa Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Oktoba 2019.

Shirika la Reli Tanzania – TRC pamoja na 'Clouds Media Group' (CMG) waadhimisha miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere kwa kufanya safari ya kihistoria kutoka Dar es Salaam kuelekea Dodoma kwa kutumia treni ya Deluxe kwa lengo la kuenzi mawazo ya Baba wa taifa ya kuhamasisha watanzania kuhamia makao makuu ya nchi jijini Dodoma kwa kutumia usafiri wa treni hivi karibuni, Oktoba 2019. Katika safari hiyo Menejimenti ya Shirika la Reli Tanzania ikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa iliungana na timu ya Clouds.. >> Inaendelea Uk. 2



## TRC YATOA KIPAUMBELE CHA MAFUNZO KWA WAHANDISI WA KIKE



>> Uk. 3

## RAIS MAGUFULI ANAVYOISHI NA NDOTO ZA BABA WA TAIFA MWL. J.K. NYERERE

Serikali ya awamu ya tano chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli imekua kipaumbele katika kuboresha miundombinu ya nchi ya Tanzania ambapo ilikua ni ndoto kubwa na mipango aliiyokuwa nayo baba wa Taifa Mwl. J.K Nyerere toka enzi za uhai wake katika kuhakikisha nchi inakua na misingi imara ya miundombinu >> Inaendelea Uk. 8

# SHIRIKA LA RELI TANZANIA NA CLOUDS MEDIA GROUP WAADHIMISHA MIAKA 20 YA MWL. NYERERE

Na Mwandishi wetu TRC >> Inatoka Uk. 1


Media Group', timu ya Tigo Fiesta pamoja na wasanii zaidi ya 200 kuelekea Dodoma kuadhimisha miaka 20 ya Baba wa Taifa lakini pia kutoa burudani kwa wananchi wa mkoa wa Dodoma.

Licha ya kujionea Vivutio kibao vya nchi yetu ikiwemo maajabu ya mto Ruvu kwenye Safari ya kihistoria kati ya CMG na TRC, timu ya Tigo Fiesta 2019 imefanikiwa kujionea utendaji kazi wa wakandarasi waliopewa dhamana na Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kujenga Reli ya Kisasa – SGR kuanzia Dar es Salaam hadi Makutupora mkoani Singida ambapo wasanii walitembelea Kilosa katika eneo ambalo handaki refu zaidi nchini linajengwa.

Katika safari hii ya kuadhimisha miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere, TRC na CMG walihakikisha uwepo wa Mwl. Nyerere ndani ya treni ambapo vitu kadhaa ambavyo vilipendwa na Baba wa Taifa vilienziwa ikiwemo mchezo wa Bao ambao alikuwa akiupenda, hotuba zake pamoja na vyakula pendwa vya Mwl. Nyerere navyo vilipikwa katika safari hiyo.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana na Ajira Mhe. Anthony Mavunde ameipongeza TRC kwa mapinduzi makubwa yaliyofanyika katika kipindi kifupi pia amefurahi kuona wasanii wengi wameingia Dodoma kwa kutumia usafiri wa treni na anaamini kwamba wasanii wamefurahi, wamejifunza mengi na watakuwa mabalozi wazuri kuhusu usafiri wa reli pamoja na Mradi mkubwa wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa kwa niaba ya Shirika amemshukuru Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kudumisha mawazo ya Mwalimu kwa kuhamishia serikali mjini Dodoma na kuboresha miundombinu ya reli ambayo ndio msingi mkuu wa usafirishaji nchini, pia amewashukuru Naibu Waziri Mhe. Anthony Mavunde, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Patrobas Katambi, timu ya CMG na wasanii kwa ujumla katika maadhimisho ya miaka 20 ya Baba wa Taifa na amesema kuwa ana imani kwamba safari hiyo iimesaidia kutunza historia kuhusu maisha ya Baba wa taifa.



*Baba wa Taifa Hayati Mwl. J.k. Nyerere (wa pili kulia) akicheza Bao enzi za uhai wake, kulia ni mkewe Mama Maria Nyerere na Rais Mstaafu wa Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mzee Ali Hassan Mwinyi wakifuatilia mchezo huo kwa makini.*




*Pichani ni Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kungu Kadogosa (mwenye shati jeupe), akicheza bao na Mtangazaji wa Clouds FM Bwana Paul James (kulia), huku Kijah Yunus akiangalia mchezo huo kwa makini walipokuwa kwenye safari ya kihistoria kuelekea Dodoma hivi karibuni, Oktoba 2019.*



*Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere akiwa katika moja ya treni zilizokuwa zikimilikiwa na Shirika la Reli Tanzania - TRC enzi za uhai wake.*

# UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR WATOA KIPAUMBELE CHA MAFUNZO KWA WAHANDISI WA KIKE 20

Na Mwandishi wetu TRC




Shirika la Reli Tanzania nchini - TRC latoa nafasi 20 za mafunzo kwa vitendo kwa muda wa miezi miwili katika Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kwa wahandisi wanawake katika hafla iliyofanyika ukumbi wa mikutano uliopo ofisi ya makao makuu TRC Dar es Salaam hivi karibuni Oktoba, 2019.

Lengo la kutoa nafasi hizo kwa wahandisi wanawake ni kuwaongezea ujuzi lakini pia kuongeza idadi ya wahandisi wanawake katika Miradi ya Shirika hususani mradi wa SGR ili waweze kujenga na kubuni miundombinu ya reli nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amesema kuwa Shirika limetoa nafasi hizo ili kuhamasisha wanawake na kuondoa dhana ya kwamba shughuli za uhandisi zinafanywa na wanaume tu na si wanawake. Amewaasa kuwa na moyo wa kulitumikia taifa lao na kuwa na uthubutu wa kufanya vitu kwa maendeleo ya taifa.

"Watu wanapopata nafasi ya mafunzo kama haya, ni dhahiri wanapaswa kuyafanyia kazi" alisema Ndugu Kadogosa.

Aidha Ndugu Kadogosa alisema kuwa TRC ni sehemu nzuri ya kupata mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wa nyanja tofauti na pia kuwasihi wahandisi hao kujenga tabia ya kufuatilia miradi ya reli katika nchi za nje kupitia mtandao ili kupata ujuzi zaidi.

Naye Msajili wa Bodi ya Wahandisi kutoka Bodi ya Usajili Wahandisi Tanzania - ERB, Mhandisi Patric Balozi amesema mafunzo haya ya vitendo kwa kundi hili maalumu la wahandisi wanawake yatasaidia kuongeza wingi wa wataalamu hapa nchini na kuacha kutegemea wataalamu wa nje.

"Watanzania wawe wazalendo kwa ajili ya kutumikia nchi yao wenyewe", alisema Mhandisi Balozi

Mhandisi Balozi ametoa shukurani kwa Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa kutoa nafasi hii na kusema kuwa wanawake wanapopata nafasi kama hizi wanatakiwa kujituma hali hii itawafanya kuwa wakakamavu na kushirikiana kwa pamoja katika maendeleo ya kujenga taifa.

"Tunawahamasisha wahandisi wa kike ili tusiwapoteze, watumie nafasi hii kujifunza waweze kuwa katika historia ya mradi mkubwa wa SGR" alisema Mhandisi Balozi.

Meneja Mradi ujenzi wa Reli ya SGR kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro Mhandisi Machibya Masanja amesema kuwa kikubwa ni juhudi katika kazi na kujifunza, pia amewakaribisha wahandisi hao kujifunza ili kuweza kuendesha miradi ya reli itakayoendelea nchini.

# SHIRIKA LA RELI TANZANIA LAADHIMISHA WIKI YA HUDUMA KWA MTEJA OKTOBA 07- 13, 2019

Na Mwandishi wetu TRC



*Afisa wa Huduma kwa Wateja kutoka Shirika la Reli Tanzania Bi. Millegrate David (Kulia) akifafanua jambo kwa wateja katika Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyofanyika katika Stesheni ya Kamata jijini Dar es Salaam hivi karibuni Oktoba 2019.*

Wiki ya huduma kwa wateja huadhimishwa wiki ya kwanza ya mwezi Oktoba kila mwaka Duniani kote, ikiwa ni sehemu ya kurudisha shukrani kwa wateja, kuwakumbusha wateja haki na wajibu wao pamoja na mtoa huduma, kuhuisha uhusiano, morari na utendaji kati ya mteja na mtoa huduma, maadhimisho hayo yamefanyika kuanzia tarehe 07 - 13 Oktoba, 2019.

TRC mpya ikiwa ni taasisi ya umma inayotoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya reli, imeadhimisha wiki hiyo ikiwa na ujumbe unaosema "JE! UMESIKILIZWA?", lengo likiwa ni kumfikia mteja moja kwa moja na kujua kama amesikilizwa na kuhudumiwa.

Katika kuadhimisha wiki hii, kitengo cha huduma kwa wateja kilishirikiana na Idara ya Maendeleo ya Biashara na Kitengo cha Habari na Uhusiano ili kuwafikia wateja wetu kwa njia ya kuwatembelea na kuzungumza nao ana kwa ana na kupitia mitandao ya kijamii. Kitengo cha huduma kwa wateja kilifanikisha mambo yafuatayo; kuanzisha Dawati maalumu kwa wiki ya Huduma kwa Wateja katika stesheni ya Kamata ambapo kiongozi wa kitengo, Kaimu wa Idara ya Uendeshaji Bw. Shaaban Kiko

Pia Shirika kupitia Kitengo cha Huduma kwa Wateja na Idara ya Biashara iliwatembelea wateja wakubwa wa mizigo katika sehemu zao za kazi kwa lengo la kusikiliza maoni, kero na malalamiko kutoka kwa wateja ili kuendelea kuboresha huduma zetu pamoja na kutambulisha kwao wazo la kutumia mabehewa ya TRC kubandika matangazo yao (Branding) ikiwa ni sehemu ya kuongeza mapato ya shirika.

Katika wiki ya huduma kwa wateja, kupitia dawati maalumu kitengo kiliweza kutoa huduma kwa abiria wa treni za bara Zaidi ya 3500 na wa treni za mjini Zaidi ya elfu 5000 waliofika kukata tiketi na kusafiri.

Pia katika wiki hiyo maofisa wa kitengo cha Huduma kwa Wateja na Huduma za Usafiri wa Abiria walifanya ziara katika Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia - TAZARA lengo likiwa ni kubadilishana uzoefu wa kazi hasa katika kuwahudumia abiria wa usafiri wa treni.

Aidha, Shirika lilitoa elimu ya uelewa kwa wateja kuhusu Haki na wajibu wao katika kupata huduma lakini pia haki na wajibu wa mtoa huduma (TRC) kwa kufanya mikutano na wateja katika stesheni ya kamata na kupitia Mitandao ya kijamii.

Shirika la Reli Tanzania linaendelea kutimiza maono yake ambayo ni kuwa Mtoa huduma bora wa usafiri wa reli Afrika Mashariki na Kati kwa kuboresha huduma za usafiri wa abiria na mizigo kupitia Miradi ya Uboreshaji wa Reli ya Kati, Ukarabati wa Mabehewa pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa.

Hivyo shirika linamthamini mteja kwa kumpa uhuru wa kutoa maoni, mapendekezo, na kueleza kelo pamoja na changamoto wanazokumbana nazo kwa kuandika maoni katika sanduku la maoni, simu ya bure, lakini pia kupitia mitandao ya kijamii, kupitia maoni kutaongeza ubora wa huduma na utendaji kazi kwa Shirika.

*Watumishi wa kitengo cha huduma kwa wateja wakiwa na Meneja Uendeshaji wa Kampuni ya BAKHRESA Dkt. Ally Saburi (kushoto), walipotembelea ofisi ya Kampuni ya BAKHRESA jijini Dar es Salaam katika maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja hivi karibuni Oktoba 2019.*



# JESHI LA POLISI TANZANIA LAENDELEA NA MIKAKATI YA KUIMARISHA ULINZI KATIKA MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu TRC



*Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Machibya Masanja (kulia) akiwalezea Makamishna na Maafisa wa Jeshi la Polisi Tanzania kuhusu maendeleo ya ujenzi wa Stesheni ya SGR inayojengwa eneo la Pugu Dar es Salaam hivi karibuni 2019.*

Makamishna pamoja na Maafisa waandamizi wa Jeshi la Polisi Tanzania wafanya ziara katika Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro hivi karibuni 2019.

Lengo la ziara hiyo ni kuona namna bora ya kuimarisha ulinzi ili kuhakikisha Miradi mikubwa ya kimkakati ukiwemo mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR unalindwa na unakuwa salama.

Makamishna na Maafisa hao walipata fursa ya kuona maendeleo ya Mradi pamoja na kazi zinazoendelea za ujenzi wa Stesheni ya Dar es Salaam, Pugu na Soga, ujenzi wa Madaraja, tuta, vivuko, utandikaji wa reli na baadae walitembelea kiwanda cha Mataruma kilichopo Soga mkoani Pwani.

Ziara hiyo imefanyika baada ya kikao kazi cha Makamishna na Maafisa waandamizi wa Jeshi la Polisi Tanzania ambapo Kamanda wa Jeshi la Polisi Nchini - IGP Simon Sirro aliwataka Makamishna na Maafisa hao kutembelea Miradi mikubwa ili kuimarisha mikakati ya ulinzi.

Akizungumza na Reli na Matukio Kamishna wa Polisi Utawala na Rasilimali Watu Kamanda Benedict Wakulyamba

amesema kuwa jukumu la jeshi la polisi ni kuhakikisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao pamoja na mali za serikali ikiwemo Miradi mikubwa ya kimaendeleo

"Miradi hii mikubwa ambayo tuna jukumu la msingi la kuhakikisha inakuwa salama na endelevu, Wajibu wetu wa kwanza ni kuhakikisha kuwa kuna ulinzi wa kutosha" alisema Kamishna Wakulyamba

Kwa upande wake Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Udhibiti Madawa ya Kulevya Zanzibar Kamanda Kheriyangu Mgeni Khamis ametoa shukurani kwa Shirika la Reli Tanzania kwa kuwapa taarifa na maelezo ya kutosha kuhusu mradi huo na amesema kuwa lengo la ziara hiyo ni kuona jinsi ya kuboresha ulinzi na usalama katika maeneo ya mradi.

"Tumekuja hapa kwenye ziara hii kuona ili tutakaporudi tuweze kujipanga kimkakati kwa ajili ya ulinzi na usalama" alisema Kamanda Kheriyangu

Naye Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Dar es Salaam – Morogoro Mhandisi Machibya Masanja kwa niaba ya Shirika la Reli Tanzania – TRC amelipongeza Jeshi la Polisi Tanzania na ameongeza kuwa Shirika limeweka mifumo ambayo haitaruhusu reli kuhujumiwa kwa kuwa reli ya kisasa itaungwa na kuwa moja (Continous Welded Rail), itawekewa na kufungwa na vifungashio ambavyo si rahisi kwa mtu kufungua na kuhujumu reli.

"Tunalipongeza jeshi la polisi kwa kuona umuhimu wa mradi, mradi huu si wa TRC ni wa watanzania, jeshi la polisi lina nafasi kubwa ndani ya mradi kwa sababu wao ndio wataalam wa ulinzi, tumebadilishana mawazo juu ya mfumo wa ulinzi na usalama tulionao katika mradi, sisi kama wahandisi tumekidhi katika kuweka mifumo ya kuhakikisha reli haihujumiwi" alisema Mhandisi Machibya

Shirika linaendelea kuhamasisha taasisi, jumuiya, makampuni na wananchi kwa ujumla kutoa ushirikiano kwa kulinda miundombinu ya reli kwa sababu miundombinu hiyo ina manufaa kwa watanzania wote, hivyo jukumu la ulinzi na usalama wa Miradi na Miundombinu ya reli ni la kila mmoja wetu.

# Huduma / Treni za TRC










*TRC ina treni ya kisasa ya Deluxe ya abiria ya kisasa inayofanya safari kati ya Dsm - Kigoma, Tabora na Mpanda. Treni ya Ordinary ambayo inafanya safari zake mara mbili kwa wiki, kutoka Dar es Salaam - Kigoma na Mwanza kupitia Tabora na kurudi Dar es Salaam. Treni hizi zina daraja la pili kulala, kukaa na daraja la tatu pamoja na behewa maalum la huduma ya chakula na vinywaji.*

*Treni mbili za mjini zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam - Ubungo na Pugu nyakati za asubuhi na jioni. Tikiti zinapatikana kwa TShs. 400 kwa treni ya Dsm - Ubungo na TShs. 600 kwa treni ya Dsm-Pugu, na TShs. 100 kwa Mwanafunzi.*

*Treni za mizigo zinafanya safari zake kupitia reli ya Kati na Tanga ambapo bidhaa mbalimbali zinasafirishwa kwenda kwa wateja wetu wa ndani ya nchi na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na nchi ya Demokrasia ya Congo kupitia Isaka, Mwanza na Kigoma.*




*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (Kulia) akimkabidhi mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa mifumo ya umeme katika Reli ya Kisasa - SGR Mhandisi Salim Mustapha wakati wa hafla fupi ya kufunga mafunzo hayo ya kifungu "I" (Package I) katika kambi ya SGR Ilala Shaurimoyo jijini Dar es Salam hivi karibuni Oktoba 2019.*



*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kati) akiwa katika picha ya pamoja na wahitimu wa mafunzo, wakufunzi kutoka kampuni ya Yapi Merkezi na baadhi ya Maofisa wa TRC katika kambi ya SSGR Ilala Dar es Salaam hivi karibuni Oktoba 2019.*



*Mtaalamu wa Masuala ya Kijamii kutoka Shirika la Reli Tanzania Bwana Leodgard Lazarus (aliyevalia kizibao cha kijani) akifafanua kuhusu taratibu za kuhamisha Makaburi kwa Wananchi wa Kata ya Makulu mkoani Dodoma hivi karibuni Oktoba 2019.*



*Maafisa wa Shirika la Reli Tanzania - TRC wakijadiliana na Viongozi wa Kata ya Makulu kabla ya kuanza zoezi la uhamasishaji wananchi kushiriki zoezi la kuhamisha Makaburi ili kupisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa mkoani Dodoma hivi karibuni Oktoba 2019.*



*Zoezi la Ulipaji Fidia ili kupisha mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Morogoro - Makutupora likiendelea katika mtaa wa Ihumwa mkoani Dodoma hivi karibuni Oktoba 2019*



*Afisa wa Shirika la Reli Tanzania Bw. Yusuph Mrisho akikabidhi hundi ya malipo ya fidia kwa Mkazi wa Kimambila Kilosa mkoani Morogoro Bi. Fatuma Ally ili kupisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Morogoro - Makutupora mkoani Singida hivi karibuni Oktoba 2019.*

## RAISI MAGUFULI ANAVYOISHI NA NDOTO ZA BABA WA TAIFA MWL. JULIUS KAMBARAGE NYERERE

Na Mwandishi wetu TRC >> Inatoka Uk. 1

hasa usafirishaji ukiwemo wa barabara, reli, usafiri wa anga pamoja na njia ya majini ili kukuza kiuchumi na maendeleo ya nchi .

Raisi Magufuli amekua na kasi kubwa ya kukuza maendeleo ya nchi kwa muda mfupi wa kipindi chake cha uongozi, ikiwemo kutekeleza mradi mkubwa wa reli ya kisasa ya SGR yenye kiwango cha reli za kimataifa ambao utaleta mabadiliko ya kiuchumi punde tu utakapokamilika, mradi huo ambao umelenga kutumia muda mfupi wa usafirishaji na kama tujuavyo kwamba muda ni mali, bila shaka wananchi hawatatumia muda wao mwingi kwenye usafiri kama kipindi cha nyuma bali watakua na muda mwingi wa kufanya shughuli za maendeleo kwa kuwa na usafiri wa uhakika.

Hayo yote yametokana na maono ya mbali ya Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere ambapo maono na uongozi wake bora umejenga misingi imara kwa maraisi na viongozi wa baada yake kufuata nyayo za kuongoza vyema nchi bila kujali imani zao na ukabila ila kujikita katika kuongoza vyema, kusimamia amani kwa wananchi pamoja na kukuza uchumi wa nchi.


Reli ya kwanza Tanzania kihistoria inaonyesha ilijengwa na Mkoloni zaidi ya miaka mia moja(100) iliyopita, ambapo reli hiyo ilijengwa mwaka 1905 na kufika Morogoro mwaka 1907, pia ikafika Tabora mwaka 1912 na kufika Mwanza 1928.

Katika ujenzi huu, Mkoloni alijenga Reli katika Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Tanga ili kuweza kutimiza azma yake ya kubeba malighafi mbalimbali zikiwemo Madini katika Mikoa ya Shinyanga na Mwanza, Mawese katika Mikoa ya Kigoma, pamoja na vibarua. Reli hiyo ya zamani ambayo ilikua na uwezo wa kuifanya treni ikimbie umbali wa kilomita 35 kwa saa , jambo ambalo limefanya treni kutumia muda mrefu njiani hali hii pia huchangia maendeleo kuwa duni, hivyo kutokana na changamoto hiyo, Rais Dkt. John Pombe Magufuli ameweka nia ya kuiboresha Reli hii ya zamani ambapo, kiasi cha Dola za Marekani Milioni 300 zinatengwa kutoka Mkopo wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuikarabati Reli hii ya zamani kutoka Dar es Salaam hadi Isaka, ikiwa na umbali wa kilomita 970, ambapo Reli yote inatarajiwa kuondolewa na haitmaye kuwekwa Reli mpya. Katika Miaka minne ya Rais Magufuli, miongoni mwa mafanikio makubwa ambayo watanzania wanapaswa kujivunia na kuamini kuwa Rais Magufuli anaishi katika ndoto za Baba wa Taifa ni pamoja na kuunganishwa kwa Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli nchini na Kampuni ya Reli nchini - TRL na kisha kuzaliwa kwa Shirika la Reli Tanzania - TRC ambayo Baba wa Taifa aliiacha, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi wa kazi katika kutoa huduma za usafirishaji wa mizigo na abiria zaidi ya ilivyokuwa awali.

Serikali ya awamu ya tano kupitia TRC imeweka juhudi za usimamizi wa ujenzi wa Reli ya kisasa – SGR ambayo ni reli ya kwanza Afrika Mashariki na Kati itakayokuwa na uwezo wa kupitisha treni zitakazoendeshwa kwa nguvu ya umeme, yenye mwendo kasi usiopungua kilometa 160 kwa saa na yenye uwezo wa kubeba mzigo wa Tani elfu kumi (10,000) kwa mkupuo. Ujenzi wa reli ya kisasa una mtandao usiopungua KM 2,561 ambao unajengwa kwa awamu tano ambazo ni Dar es Salaam hadi Morogoro km 300, Morogoro hadi Matukupola Km 422, Matukupola hadi Tabora km 294, Tabora hadi Isaka km 130, Isaka hadi Mwanza 249.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye rasimali nyingi ambazo serikali kwa namna moja ama nyingine imeamua kuwekeza nguvu nyingi katika kuhakikisha rasilimali hizo zinavunwa kiufasaha kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho na kupelekea kuyaenzi maono ya baba wa taifa Mwl. J.K. Nyerere kwa matendo kupitia kauli na ushauri aliokuwa akiutoa.

*KUMBUKUMBU*
*Pichani ni Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa na Treni ya Rais Miaka ya 1960 kabla ya Uhuru wa Tanganyika.*



# MAHANDAKI YATAKAYOPITISHA RELI YA KISASA MKOANI MOROGORO KUWA KIVUTIO CHA UTALII

Na Mwandishi wetu TRC



Usafiri wa Treni ni moja ya aina ya usafiri wa kipekee ambao huifanya safari kuwa zaidi ya safari kutokana na vitu kadhaa ambavyo msafiri anaweza kuvipata endapo atatumia usafiri huo. Tunaposema "safari kuwa zaidi ya safari" tunamaanisha kwamba lengo kuu la msafiri ni kufika aendako lakini unaposafiri na treni utafika uendako kwa haraka lakini pia utapata fursa ya kutalii kwa kujionea vivutio tofauti vilivyopo sambamba na njia ya reli, utapata fursa ya kutembea yaani kuhama behewa moja hadi jingine, utapata huduma ya chakula na vinywaji, huduma ya matibabu ya awali (First Aid), vyumba vya kupumzika, kutazama luninga bila kusahau picha za kumbukumbu.

Usafiri wa treni umekuwa ukitumika sana kwa abiria na wafanayabiashara wanaosafirisha bidhaa zao kwa umbali mrefu, lakini hivi sasa suala la umbali si sababu inayowafanya wengi kutumia treni, bali hii inatokana na mabadiliko ya teknolojia ambayo yamepelekea usafiri wa treni kuwa miongoni mwa usafiri wa haraka, usio na foleni wala bugudha yoyote kutokana na kuwepo na treni ziendazo kasi zaidi ambazo pia zimekuwa vivutio duniani.

Kivutio kingine kikubwa katika usafiri wa reli ni Mahandaki 'Tunnels' ambayo yanachorongwa katika maeneo yenye Milima mirefu au miinuko mikali. Handaki 'Tunnels' ni njia ya chini ambayo hujengwa kwa kuchoronga mlima ili kupitisha barabara, reli, njia za watembea kwa miguu, mabomba na miundombinu mingine pia hutumika kama sehemu ya kujihifadhi wakati wa vita. Mahandaki yanatajwa kutumia gharama nafuu zaidi kuliko ujenzi wa Madaraja na Pasua 'Open Cuts' katika maeneo yenye miinuko lakini pia ujenzi wa mahandaki hutegemea sana aina ya miamba na udongo wa eneo husika.

Mahandaki katika usafirishaji hujengwa ili kukidhi mahitaji ya uchukuzi kutoka sehemu moja kwenda nyingine katika maeneo yenye vikwazo ikiwemo miinuko mikubwa. Katika Makala hii tutajikita zaidi katika Mahandaki yanayojengwa ili kupitisha reli hususani katika Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Morogoro hadi Makutupora Singida.

Hapa Tanzania Handaki refu linapatikana katika reli ya TAZARA lina urefu wa Mita 873, lakini katika Mradi wa SGR kipande cha Morogoro – Makutupora katika Mahandaki manne (4) yanayojengwa kutakuwa na handaki refu zaidi lenye urefu wa Meta 1031 sawa na Kilometa 1.031, kukamilika kwake kutaleta chachu katika sekta ya usafiri wa reli na utalii.

Katika Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR kipande cha Morogoro – Makutupora jumla ya Mahandaki manne (4) yatajengwa huku Handaki la kwanza litakuwa na urefu wa Mita 424, la pili litakuwa na urefu wa Mita 1031, handaki la 3 Mita 820 na la mwisho litakuwa na urefu wa Mita 380, Mahandaki haya yote yataunganishwa na Madaraja ili kuepuka athari za mto Mkondoa amabo umekuwa ukiathiri huduma ya usafiri wa reli ya kati ambapo mara nyingi Shirika hulazimika kusitisha huduma kwa muda kwa kipande cha Kilosa hadi Gulwe ili kupisha ukarabati kutokana na athari za mafuriko ya mara kwa mara katika kipindi cha mvua.

Mahandaki hujengwa pale inapobidi kuwepo kwa usafiri wa haraka ambao hauhitaji vikwazo au muingiliano na kitu kingine, kufupisha njia ya safari, kwani mara nyingi haihitaji kutwaa ardhi kwa ajili ya miundombinu. Wataalamu wanasema zipo njia nyingi za Uchorongaji na Ujenzi wa Mahandaki kulingana na hali ya ardhi ya eneo husika, lakini njia nzuri inayotumiwa na wataalamu wengi katika ujenzi wa Mahandaki ni kuchimba na kuripua, njia hii ni salama na nafuu zaidi. Njia hii pia inatumika katika ujenzi wa Mahandaki yatakayopitisha reli ya SGR kipande cha Morogoro - Makutupora.

"Uchorongaji wa Handaki letu unahusisha njia inayoitwa 'Drill and Blast' yaani kuchoronga na kuripua, njia hii ni mahususi katika uchimbaji wa Mahandaki hasa mwamba unapokuwa mgumu pia haitumii gharama kubwa, njia hii inahusisha utoboaji wa matundu katika uso wa handaki, kujaza Miripuko katika uso wa Handaki na kuripua. Mara baada ya kuripua tunapeleka hewa ya kutosha ndani kwa ajili ya kuondoa vumbi, gesi pamoja na sumu ili wafanyakazi waliopo katika maeneo haya wawe katika mazingira salama ya kufanya kazi ya uondoaji kifusi" alisema Mhandisi Amir Khamis Mshauri wa Mahandaki KORAIL

Ubora wa malighafi na vifaa vinavyotumika katika Ujenzi wa Handaki ni kitu muhimu cha kuzingatia ili kuhakikisha Handaki linakuwa sehemu salama na rafiki wa Mazingira katika eneo husika. Wahandisi wanazingatia viwango vya ubora wa kimataifa vinavyotumika katika ujenzi wa mahandaki duniani kote. Mtaalamu Catherine Kipeli amezungumza na Gazeti hili na kueleza namna wanavyozingatia ubora wa zege linalotumika katika ujenzi wa Mahandaki hayo.

"Kazi yetu kubwa kwenye Handaki ni kupima ubora wa zege, tunapima jotoridi, na jinsi zege linavyomwagika (slamp), kwa hiyo ni lazima 'Consultant' awepo ili kuthibitisha kwa pamoja joto la hewa na jotoridi la zege, baada ya kujiridhisha tunaruhusu gari kumwaga

Inaendelea Uk. 10

Inatoka Uk. 09

zege ndani ya Handaki" alisema Bi. Catherine Kipeja, Mtaalamu wa Ubora wa kazi katika ujenzi wa handaki

Katika uchorongaji na Ujenzi wa Mahandaki zipo changamoto kadhaa ikiwemo changamoto ya maji hususani nyakati za mvua. Katika kuhakikisha maji hayasumbui katika uchorongaji wa Handaki, katika hatua za awali wahandisi huandaa mfumo wa mifereji ambao huitwa 'primary drainage system' maalum kwa ajili ya kuyakusanya na kuyapitisha maji yanayotoka juu ya mlima au muinuko ambao unachorongwa na kuyasafirisha hadi sehemu salama.

Katika hatua nyingine wahandisi huandaa mfumo wa mifereji unaofahamika 'secondary drainage systems' ili kuzuia athari zinazoweza kusababishwa na maji ndani ya handaki. Wataalamu hujenga mifumo ya mifereji juu, pembezoni, na katika kitako cha Handaki yaani 'base course drainage' ili kuhakikisha maji yanatoka nje ya Handaki kwa urahisi.

Ili kuhakikisha Handaki linakuwa sehemu salama kwa binadamu wataalamu huweka mifumo ya kisasa kwa ajili ya kuhakikisha hewa safi, salama na ya kutosha inaingia kwenye Handaki muda wote, wataalamu hujenga midomo ya kuingilia 'Entrance Portal' na mlango wa kutokea 'Exit Portal', moja ya kazi ya Midomo ya kuingilia na kutokea hutumika kwa ajili ya kupitisha hewa kuingia na kutoka ndani ya Handaki, pamoja na huweka miundominu ya umeme ambayo inahakikisha Handaki linakuwa na mwanga wa kutosha.

Ujenzi wa Mahandaki kwa ajili ya kupitisha reli au barabara ni gharama kwa namna moja, ni Miradi iliyozoeleka kuonekana katika nchi zilizoendelea hususani huko Bara Ulaya na Amerika ambako kuna hitaji kubwa la usafiri wa haraka kutokana na idadi kubwa ya watu na shughuli nyingi za kiuchumi zilizosababishwa na ukuaji wa miji hiyo.

## SERIKALI INAVYOJALI WANANCHI KWA KUWALIPA FIDIA ILI KUPISHA MRADI WA SGR.

Na Mwandishi wetu TRC

Fidia ni malipo yanayotolewa kwa mtu au taasisi kama mbadala wa mali yake kuondolewa katika eneo lake lililotwaliwa kwa matumizi mengine yenye manufa kwa umma. Sera na Sheria ya ardhi inasema kuwa ardhi ya Tanzania ni mali ya umma hivyo taratibu za kisheria hufuatwa wakati wa kutwaa ardhi, na serikali inawajibika kulipa fidia.

Suala la fidia hapa nchini si kitu cha kuepukika hasa katika awamu hii ya tano inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kulingana na uhitaji mkubwa wa ardhi kwa ajili ya miradi mikubwa ya kimkakati kwa maendeleo ya taifa.

Shirika la Reli Tanzania – TRC linaendelea na zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa reli ya kisasa – SGR Morogoro – Makutupora.

Maelfu ya wananchi wanaendelea kupokea fidia zao ambazo zitasaidia kubadilisha na kuboresha maisha yao kutokana na kwamba fedha hizo zinapotolewa, viongozi wa ngazi ya kata mpaka mkoa hutoa elimu ya matumizi sahihi ya fedha hizo katika kuleta maendeleo ya familia zao na taifa.

Fidia hiyo inahusisha rasilimali ambazo ni pamoja na ardhi, nyumba, miti ya mazao sambamba na vifuta machozi kwa ajili ya wenye Makaburi ya ndugu zao. Zoezi limeendeshwa na maafisa wa TRC wakishirikiana na viongozi wa eneo husika huku zoezi likisimamiwa na vyombo vya usalama kuhakikisha usalama wa raia na mali zao.

Akizungumza na Mwandishi wa Gazeti la Reli Matukio Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa, amesema kuwa suala la fidia ni la kisheria hivyo hakuna mwananchi ambaye hatalipwa fidia kutokana na rasilimali yake iliyotwaliwa ili kupisha ujenzi. "Kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu tutawalipa wananchi wote ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa reli hii" Mkurungenzi amesisitiza kuwa wananchi wote watafanyiwa tathimini ya mali zao na kulipwa kwa haki na usawa.

Viongozi wa vijiji walitoa neno juu ya zoezi la fidia, Bi. Beatrice Shayo ni Mtendaji wa Kijiji cha Kimambila amewapongeza maafisa wa Shirika la Reli kwa kuendesha zoezi kwa muda sahihi na kwa ufanisi huku amani na usalama ukiwepo eneo la tukio, hata hivyo amewaomba wananchi kutumia fedha kwa maendeleo ya familia zao na kijiji kwa ujumla hasa kujenga nyumba bora na za kisasa pamoja na kuanzisha biashara ambazo zitainua uchumi wa familia mpaka ngazi ya kijiji.

"Ninawaomba wanakijiji waliolipwa fidia wakazigeuze fedha hizi kuwa chachu ya maendeleo katika kuboresha maisha kwa kujenga nyumba bora na imara lakini pia kuanzisha biashara ili ziwaongezee kipato na kukuza uchumi wa familia na kijiji" Bi. Beatrice alisema.

Nao wananchi wametoa pongezi na shukurani kwa Serikali kwa kutimiza ahadi ya kulipa fidia kwa wakati huku wakiendelea kufurahia mradi huo kwani umekuwa fursa kwa wakazi wa maeneo hayo ambapo vijana wamejipatia ajira mbalimbali huku wengine wakijikita katika fursa ya biashara ndogondogo.

Mzee Adriano Hamis ni mkazi wa kata ya Kasiki Wilaya ya Kilosa Mkoani Morogoro amebainisha kuwa "mradi huu kwetu bado una fursa nyingi ukizingatia umepita wilayani kwetu, tunaweza kufanya biashasa na vijana watapata ajira za kutosha na mpaka sasa wapo vijana hawakuwa na kazi lakini sasa wanafaidika na mradi huu lakini kwa taifa ni fursa kwa kukuza uchumi wa Taifa letu".

# JE, UNAJUA UMUHIMU WA KUZINGATIA TARATIBU ZA KIAFYA KATIKA MAENEO YA KAZI?

Na Dkt. Apolinary John



Ndugu wapenzi wa gazeti letu la Reli na Matukio. Napenda kuwasalimu wale wote wafanyakazi wenzangu na wapenzi wa habari za kiafya.

Leo tutazungumzia mambo yanayohusu afya katika maeneo yetu ya kazi kwa ujumla. Haya tutakayojifunza hapa si kwa watu wa miradi kama hii ya ujenzi peke yake hapana bali hata kama ni katika ofisi yako mwenyewe, kwa aliyejiajiri (mjasiriamali). Kimsingi kuna magonjwa yanayoweza kuwapata watu kulingana na mazingira yao ya kazi yalivyo na vitu vyote vinvyozunguka maeneo yao ya kazi, kitaalamu huitwa Ergonomics.

Kila mfanyakazi hukutana na utawala au uongozi, mazingira ya kitengo chake au idara fulani, vitendea kazi na la mwisho kabisa ni majukumu yake ya kila siku ambayo hupangiwa na kiongozi wake. Kwa kawaida mtu huzaliwa, hupata matunzo yote kutoka kwa wazazi au walezi. Muda mwingi wa masomo wengine huwa mbali na wazazi wao kasoro muda ule wa likizo. Huko pia kuna mengi katika masomo, kuanzia safari, chakula, malazi na michezoni.

Kama tuliweza kuithamini afya ili tuweze kufanya vizuri katika masomo yetu. Basi ili tuweze kupata kipato chetu baada ya kuajiriwa ni lazima tuendelee kuithamini afya vilevile. Baada ya kupata ajira masaa 8 mpaka 12 kujumlisha na ule muda wa kwenda na kurudi nyumbani muda mwingi zaidi tunahesabika kuwa kazini. Kazi ndio maisha. Kiwango cha kazi kinabashiri ni hadhi gani ya maisha unakuwa nayo.

Tukiangalia afya zetu, kazi zinaweza kutupelekea kujua kuwa kulingana na nguvu tunazozitumia kila siku ni kwa muda gani tunaweza kuathirika kutokana na mazingira yetu ya kazi. Tukianza na utawala, ni lazima kuwe na mfumo mzuri wa kiutawala katika mazingira ya kazi. Hapa tunaangalia mikataba yenye kuangalia weledi wa mtu na mshahara wake. Kitu kingine ni mazingira ya kazi. Usalama kwanza na kazi baadae.

Kama mazingira hayatoruhusu mfanyakazi kuendelea kuwa salama baada ya kazi basi ni bora kazi hiyo isitishwe. Hapa watu wa usalama maeneo ya kazi ni lazima kuendelea kutoa elimu ya namna bora ya kufanya kazi katika mazingira ya kila siku au katika mazingira mapya. Kazi ya ujenzi wa reli si sawa na ujenzi wa ghorofa, hii hi kazi kubwa sana tena yenye kutambaa kutoka eneo moja kuelekea jingine.

Vipo baadhi ya vitendea kazi ambayo ni lazima kuvitumia kwa muda mchache ili kuepuka madhara mfano utumiaji wa vifaa vyenye kutoa sauti kubwa na mitetemo katika mwili. kama hakutakuwa na uangalizi mzuri basi watu wanaweza kupata madhara ya muda mfupi au ya baadae. Wapishi - jengo la kupikia ni lazima kuwa refu na lenye kuruhusu hewa kupita. Joto likizidi sana wahudumu hasa wa kiume wanaharibu mbegu zao za kiume na kuweza kuwaletea madhara ya uzazi, aidha ni muhimu kuwepo na hewa za kutosha katika maeneo ya kazi.

Kuwapatia wafanyakazi maski ili kulinda mapafu yao ni muhimu sana katika mazingira ya kazi binadamu sio mitambo au mashine ninashukuru kuona Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania inasimamia hili. Kazi inaweza kuwa nyepesi lakini mpango wa kazi unaweza ukapelekea kazi kuwa ngumu.

Hali kama hiyo inapoteza ufanisi unapotea na kuleta madhara makubwa katika akili, na hupelekea msongo wa mawazo au sonona. Muda wa mapumziko au likizo na ruhusa kwa mujibu wa sheria ni vema kuzingatiwa. Hapa inaweza kuwa ngumu kwani kisheria baba, mama, mke na mtoto ndio wanaotambuliwa lakini kulingana na tamaduni zetu shangazi, mjomba bibi na babu ndio huenda wakawa ni watu wa karibu kuliko ilivyo kawaida. Hivyo katika mambo ya uongozi kuwapa wafanyakazi uelewa wa kisheria ni muhimu ili kuepuka ugomvi usiokuwa wa lazima.

Afya ni utajiri lakini afya ni kuwa vizuri kiakili, kimwili na kijamii pia, hivyo mtu yoyote akiathirika katika sehemu mojawapo huweza kupelekea kuharibu mahusiano mema kazini.

Kampuni ya Yapi Merkezi inatoa bima ya afya ya NHIF inayowapa wafanyakazi usalama na familia zao. Wapo wahudumu wa afya kila kambi na wapo wataalamu waliobobea katika mambo ya kijamii ili kutatua migogoro na baina ya wafanyakazi na wenyeji wa mazingira ambayo mradi unapita. Mpaka sasa naona tunakwenda vizuri.

Watanzania wanazidi kutambua faida za miradi hii mikubwa ya kimkakati na kuzidi kuwa na moyo wa kizalendo zaidi na kuweza kufanya kazi vizuri usiku na mchana. Wahudumu wa afya, kazi yetu kubwa ni kukagua na kulinda afya za wafanyakazi wote kabla, baada ya ajira na hata pale watu wanapomaliza mikataba yao . Afya ni mtaji katika kazi, taifa linategemea nguvukazi ya vijana. Taifa lenye vijana wenye afya ni mwanzo mzuri wa kujenga taifa lenye maendeleo endelevu. Tunawajibu wa kulinda afya za wafanyakazi wote ili kuelekea Tanzania ya uchumi wa viwanda.

## Neno kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu



Ndugu Masanja Kungu Kadogosa
Mkurugenzi Mkuu TRC

Katika kuadhimisha miaka 20 ya kumkumbuka Baba wa Taifa Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere, Shirika la Reli Tanzania - TRC limejifunza mengi kupitia uongozi na uwepo wake kipindi hicho kwa kuweza kusimamia misingi imara ya ujenzi wa nchi hususani katika ujenzi wa miundombinu ikiwemo reli ambayo imekua ikitunzwa miaka mingi na mpaka sasa, chini ya serikali ya awamu ya tano miundombinu ya reli imeendelea kuboreshwa pamoja na kujenga reli mpya ya kisasa.
Hakika tutaendelea kumuenzi Mwl. Nyerere kwa kuishi na kufuata maelekezo na ushauri ambao ulikua na maono ya mbali katika kukuza na kuendeleza uchumi wa nchi ya Tanzania. Naamini kuwa Ujenzi wa Reli ya kisasa ya SGR utaleta maendeleo makubwa hasa kibiashara na utalii sababu hatutapoteza muda mwingi katika shughuli za uchukuzi. Ninampongeza Raisi wetu Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya vyema na kuhakikisha miundombinu ya nchi inakua imara na yenye hadhi ya kimataifa.

SHIRIKA LA RELI TANZANIA
Mtaa wa Reli/Barabara ya
Sokoine
S.L.P 70364
Dar es Salaam
TANZANIA
Barua pepe; info@trc.co.tz
Tovuti; trc.co.tz
Simu ya Bure; 0800 110 042

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| | |
|---|---|
| MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk |
| MHARIRI MSAIDIZI | Mohammed Mapondela |
| MTAYARISHAJI | Sami Omary |
| MAKALA | Aziza Charles |
| HABARI | Tracylinda Nganga |
| PICHA | Seleman Kadiko |